**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule; 0621124217 / 0756434762**

**Makamu Mkuu wa Shule;0622462549**

**Shule ya Sekondari KIMULI**

**S.L.P 36 KYERWA.**

**Tarehe 04/04/2024.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ........................................................**
**.............................................**
**S.L.P ....................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMULI HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA MKOA WA KAGERA MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya **HKL, HGFa au HGLi**

Shule ya Sekondari Kimuli ipo umbali wa Kilometa 12 Kaskazini mwa Mji mdogo wa NKWENDA. Usafiri wa Tax au hiace kutoka mjini mdogo wa Nkwenda unapatikana katika kituo cha mabasi Nkwenda. Nauli ni Shilingi 4000/= kwa pikipiki na magari.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/7/2024** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **1/07/2024**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/7/2024**.

**Wanafunzi wanashauriwa kufika mapema kwani masomo yataanza mara moja pindi shule itakapofunguliwa.**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili **dark blue** kwa Wavulana zisizo bana zisiwe modo ziwe na linda mbili mbele na nyuma mfuko mmoja tu.

ii. Mashati mawili **right blue** mikono mirefu

iii. Sare ya Michezo ni track suit ya right blue(blue bahari) na raba za michezo/ viatu vya michezo**.(VIATU VYA KUCHEZEA MPIRA WA MIGUU NI MUHIMU KWA KILA MWANAFUNZI).**

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi tatu nyeusi

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta dark blue kwa atakaye kosa zinapatikana kwa Mzabunii na **zina nembo ya shule kwa** Tshs 17,000/=

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) T-shirt blue na suruali damu ya mzee isiyo ya kubana yaani isiwe modo

ix. Tai ya dark blue yenye michilizi myeupe kwa atakayekosa inapatikana kwa Mzabuni na ina **nembo ya shule kwa** Tshs 4,000/=

x. Tisheti (T-shirt) ya blue kwa atakayekosa inapatikana kwa kwa Mzabuni na **ina nembo ya shule kwa** Tshs 12,000/=

***Agalizo fedha za sweta,Tai na T-sheti zitalipwa kwa mzabuni husika na sio benki kwa yule atakayekuwa amevikosa mahali anapotoka.***

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 10 counter books qr 4

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi MBILI (2) kwa mwaka

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika; Advanced English language 1, Advanced English language 2, Advanced History 1, Advance History 2, Kiswahili 1 Kidato cha Tano na Sita na Kiswahili 2 kidato cha Tano na Sita na Advanced Geography 1, na Advanced Geography 2.

iv. Godoro inch 2.5
v. Mashuka Jozi 2 blue blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 1 kubwa iliyoisha mafuta na ndogo 1 (lita Kumi) zenye mifuniko na beseni 1
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule yenye jina Kimuli Sekondari Revenue 31901100060 NMB.**

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumiwa na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

***DANIEL J. KIFIGO***

***MKUU WA SHULE***

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0621124127 AU 0756434762**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0758660306 AU 0622462549**
- **Mwandamizi Taaluma 0763086132**
- **Mwandamizi Malezi 0621099061**

OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA-MKOA WA KAGERA
SHULE YA SEKONDARI KIMULI
S.L.P 36,
KYERWA.

**FOMU MAALUMU KWA MWANAFUNZI**.

1. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI;
   i. Jina la mwanafunzi ………………………….. jinsi………. Tarehe ya kuzaliwa…………
   ii. Shule ya Sekondari aliyotoka…………………………………………
   iii. Jina la baba……………………........... kazi yake……………………….. Na.ya simu……………..
   iv. Jina la mama…………………………………kazi yake………………….. Na. ya simu……………..
   v. Kijiji /mtaa wanapoishi………………………. Wilaya…………………mkoa ………………………
   vi. Dini……………………..
   vii. Majina ya ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutoa msaada pindi wanapohitajika
      a. ………………………………………….. Anakoishi…………………………… Na. ya simu…………………
      b. …………………………………………... Anakoishi………………………….. Na. ya simu…………………
      c. ……………………………………………. Anakoishi………………………….. Na. ya simu…………………
      d. ……………………………………………. Anakoishi………………………….. Na. ya simu…………………
   viii. Michezo anayoweza kushiriki mwanafunzi shuleni
   ……………………………,……………………………,……………………………,……………………………

NB: Je wazazi wote wako hai ? . Ndiyo/ Hapana (Kata isiyositahili)
Kama amefariki /wamefariki aliyefariki ni………………………………………………………………

2. **KUKUBALI NA KUTII SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**.

Mimi (jina la mwanafunzi)……………………………………………………...naahidi sitashiriki kabisa katika fujo/migomo na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine .Pia naahidi kuzifuata taratibu na sheria zote za shule kwa faida yangu binafsi, shule na Taifa kwa ujumla .Endapo nitakwenda kinyume na taratibu na kanuni za shule nakubali kufukuzwa shule, kusimamishwa masomo na kufikishwa mahakamani au kupewa adhabu nyingine kulingana na sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na au sheria ya makosa jinai ya mwaka 2002

JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………. SAINI…………………………….TAREHE………………
JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………...SAINI…………………………….TAREHE……………...

3. **MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA MICHANGO NA KUTEKELEZA MAELEKEZO YA SHULE.**

Mimi (Jina la mzazi/mlezi)………………………………………………... nakubaliana na sheria , kanuni, kulipa michango yote kwa wakati muafaka na kutekeleza maelekezo yatolewayo na shule. Vilevile , naahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa uongozi wa shule pindi nikihitajika kuhusu tabia, mwenedo au suala jingine lolote linalomhusu mtoto wangu na maendeleo ya shule kwa ujumla.

JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………. SAINI……………………...TAREHE……………..

**………………...**

**DANIEL J. KIFIGO**
**MKUU WA SHULE.**

OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA-MKOA WA KAGERA
SHULE YA SEKONDARI KIMULI
S.L.P 36
KYERWA.

FOMU YA KUPIMA NA KUJUA AFYA YA MWANAFUNZI.
MGANGA MKUU/MFAWIDHI,
KITUO CHA AFYA/HOSPITALI
…………………………………..
………………………………….
…………………………………

**YAH: <u>KUJUA AFYA YA MWANAFUNZI KWA AJILI YA KUJIUNGA NA SHULE.</u>**

Kijana………………………………………. Amechanguliwa kujiunga kidato cha (v) katika shule ya sekondari KIMULI. Naomba uthibitishe hali ya afya yake kabla hajaanza masomo rasmi hapa shuleni.
Na endapo atapatikana na tatizo lolote tunaomba utujulishe , na atakapopatikana na tatizo la uoni hafifu hana budi kujinunulia miwani kwa gharama zake mwenyewe.

Kwa
MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KIMULI
S.L.P 36,
KYERWA-KAGERA

YAH: AFYA YA……………………………………………………………………….

Nimempima mtajwa hapo juu na kuthibitisha kuwa anasumbuliwa/hasumbuliwi na magonjwa yafuatayo:-

1. TB……………………………………………
2. HB……………………………………………
3. STOOL………………………………………
4. URINE………………………………………
5. EYE & EAR………………………………..
6. ATHMA………………………………………
7. THYPHOID…………………………………
8. OTHER……………………………………...

Maoni ya Daktari/Mganga mfawidhi………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………….

JINA LA DAKTARI /MGANGA MFAWIDHI                    SAINI & MHURI